**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI**

Simu:+255 26 2324455
FAX: +255 26 2323233
Barua pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mow.go.tz

Mji wa Serikali Mtumba,
S.L.P. 2888,
**40470 DODOMA.**
TANZANIA

**DODOMA,**

**26 Novemba, 2025**

## TAARIFA KWA UMMA

## HATUA ZILIZOCHUKULIWA BAADA YA ZIARA YA WAZIRI WA UJENZI, MIZANI YA MIKESE – MOROGORO

Wizara ya Ujenzi inapenda kuutaarifu umma kuhusu hatua zilizochukuliwa kufuatia ziara ya Waziri wa Ujenzi, Mhe. Abdalah Ulega alipokagua mizani ya Mikese, mkoani Morogoro tarehe 22 Novemba, 2025 na kubaini uwepo wa uzembe wa kutoshughulikia kuharibika kwa mizani ya kupima magari yakiwa kwenye mwendo (WIM) na kusabisha foleni katika barabara kuu ya Dar es Salaam - Morogoro.

Kutokana na hali hiyo, Mhe.Waziri Ulega alitoa maelekezo ya kurejeshwa kwa huduma ya mizani hiyo haraka na kusimamishwa kazi kwa watumishi waliohusika na uzembe huo.

Maelekezo ya Waziri Ulega tayari yamefanyiwa kazi na Wizara, ambapo timu maalum ya wahandisi na wataalamu wa mizani imeanza kufanya matengenezo ya mifumo yote ikiwemo mfumo wa kupima magari yakiwa kwenye mwendo (Weigh in Motion) kuanzia tarehe 25 Novemba, 2025, ili kuhakikisha mizani inarejea kufanya kazi kwa ufasaha na kwa viwango vinavyokubalika kitaifa na kimataifa.

Aidha, wasimamizi watatu (03) waliohusika na uzembe huo wamesimamishwa kazi ili kupisha uchunguzi. Wasimamizi hao ni pamoja na Meneja wa mizani kutoka Wakala ya Barabara Tanzania (TANROADS), Makao makuu, Eng. Leonard Mombia, Meneja wa TANROADS Mkoa wa Morogoro, Eng. John Mkumbo na Msimamizi wa mizani Mkoa wa Morogoro, Eng. British Mpeli.

Wizara inawahakikishia wananchi kuwa wakati ukarabati ukiendelea, utaratibu maalum umewekwa na unasimamiwa kwa weledi ili kuhakikisha magari yanaendelea kuhudumiwa kwa kufuata sheria za usafirishaji bila usumbufu.

Imetolewa na;
Katibu Mkuu,
Wizara ya Ujenzi